# Mwanamke wa Kisasa katika Insha za Kifasihi Magazetini: Mtazamo wa Nadharia ya Upalizi

*Moses Wamalwa Wasike*
*Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya*
*mwasike@gmail.com*

## Ikisiri

Magazeti yana mchango mkubwa katika kuifahamisha jamii kuhusu masuala mbalimbali yanayoiathiri. Makala yanayochapishwa magazetini huwawilisha ujumbe kutoka kwa waandishi hadi kwa hadhira ya wasomaji kupitia njia mbalimbali kwa nia ya kuathiri mitazamo na mielekeo yao kuhusu masuala ya kijamii. Mbali na matumizi ya lugha ya kawaida, lugha ya kifasihi kutumika katika baadhi ya makala ili kuhamasisha wasomaji. Mojawapo ya makala hayo ni insha za mienendo za 'Staffroom Diary' zinazoandikwa na Frankline Muyonga ambaye ni maarufu kwa jina la Mwalimu Andrew katika gazeti la Sunday Nation, Kenya; The Citizen, Tanzania na Daily Monitor, Uganda. Masuala yanayoangaziwa katika makala haya na aghalabu kwa mseto wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili kwa mtindo wa ucheshi ni ya kisiasa, kijamii na kitamaduni. Ingawa insha hizi zimekuwa zikichapishwa tangu mwaka 2009, uchunguzi wa kina haujafanywa kuhusu jinsi zinavyowachora wanawake na athari zake kwa mitazamo na mielekeo ya wasomaji kuhusu jinsia hii. Azma kuu ya makala haya ni kubainisha kasumba au usaguzi chanya (positive stereotypes) unaosindikizwa kwa hadhira katika insha hizi kwa misingi ya Nadharia ya Upalizi (Cultivation Theory) iliyoasisiwa na George Garbner (1969). Mtazamo huu huchunguza athari za vyombo vya habari kwa mitazamo ya hadhira yake kuhusu masuala ya kijamii yakiwamo ya jinsia. Umejikita katika wazo kwamba hatimaye watu huja kuamini wanayoyaona, kusikia au kusoma kwenye vyombo hivi kuwa ni fumano la ukweli au uhalisia wa maisha. Uchunguzi wetu umetalii jinsi mwanamke anavyosawiriwa na jinsi makala haya yanavyojenga mitazamo miongoni mwa wasomaji. Nakala teule za makala ya 'Staffroom Diary' pamoja na uchunguzi wa maandishi mbalimbali kuhusu mada hii zimetumiwa kama vyanzo vya data ya utafiti huu. Wasomaji wapenzi wa insha hizi watapata ukweli kuhusu nafasi ya mwanamke katika insha hizi mintarafu ya hali halisi. Halikadhalika, watafiti wa Kiswahili watatumia matokeo ya uchunguzi huu kutafitia zaidi vipengele vingine vya insha za kifasihi katika magazeti.

## 1.0 Utangulizi

Mkabala wa kuumeni umetawala jamii nyingi za kilimwengu kwa muda mrefu. Suala hili limesababisha kupuuzwa kwa haki za wanawake kama viumbe kamili. Kauli za kidini na kitamaduni zimetumiwa kushadidia uwezo wa wanaume na kuwadunisha wanawake. Kwa mujibu wa Engels (1884) mabadiliko yaliyotokea na yenye ustaarabu ndiyo yaliyosababisha udhalimu dhidi ya wanawake. Jamii asilia ilikuwa na uthamini sawa wa kazi za wanaume na wanawake. Baadaye mabadiliko ya ustaarabu yalianzisha urithi wa upande wa baba. Haya yalitokana na mazingira ambapo kazi za wanaume za uwindaji na ufugaji zilipoanza kuleta faida zaidi kuliko kazi za nyumbani. Ongezeko la mali upande wa baba ni suala lililozusha kuwapo kwa mali ya kibinafsi na hivyo wanawake wakaanza kuwategemea wanaume kiuchumi. Ukandamizwaji wa wanawake katika jamii unatokana na mfumo unaodhibitiwa na wanaume (Momanyi, 1998). Momanyi anadai kuwa mifumo ya kuumeni ni utaratibu mkubwa wa masharti ambao unachukuliwa kumaanisha kule kuhalisishwa kwa asasi za kijamii zenye kuhimili tofauti za kiuana katika ugawaji wa kazi. Huu ni mfumo ambao unampa mwanamume nguvu dhidi ya mwanamke katika nyanja zote za kimaisha. Katika ugawaji wa majukumu chini ya mfumo huu, wanawake wanapewa nafasi ya pili, baada ya mwanaume.

Ripoti ya uchunguzi ya World Economic Forum (Global Gender Gap Report, 2016) inaonesha kuwa katika ulimwengu kuna mataifa machache sana ambayo yametimiza usawa wa kijinsia katika sekta za elimu, afya, uchumi na siasa. Wanawake wanakandamizwa na kubaguliwa na nguvu zinazobainishwa kuwa: umaskini, kauli na shughuli za kidini na kitamaduni hasa ubabedume unaodhihirika kupitia mfumo unaoegemea kuumeni.

### 1.1 Harakati za Kumkomboa Mwanamke

Upembezwaji au utelekezwaji huu umevyaa mvuvumko kote ulimwenguni wa kumkomboa mwanamke. Mathalani, Kenya kumekuwa na juhudi katika bunge la kumi na moja, za kushinikiza kutekelezwa kwa mswada wa kikatiba wa usawa wa kijinsia utakaompa mwanamke uwakilishi sawa na wa mwanamume katika nyadhifa za uongozi. Ulimwenguni kote zipo juhudi za kumwezesha mwanamke kukuza ukakamavu, ujasiri na nafasi yake kwa kumwondolea mikatale ya kasumba hasi zinazomdunisha.

Pia, kuna jitihada za kubadilisha jinsi wanawake wanavyosawiriwa katika vyombo vya habari ambavyo hufinyanga kwa kiasi kikubwa maoni, mielekeo

na mitazamo kuhusu masuala ya kijamii. Ni kutokana na ukweli huu ndipo Kongamano la Tano la Wanawake Ulimwenguni kote *(Fourth World Conference on Women)*, Beijing 1995 lilipotambua nafasi kuu ya vyombo vya habari katika kuleta usawa. Azimio likawa kubadilisha jinsi vyombo vya habari vinavyosawiri wanawake *(Platform for Action)* likaafikiwa (Gallagher, 1995).

Kufuatia utambuzi kuwa vyombo vya habari vina uwezo mkubwa wa kubadilisha mitazamo ya jamii kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii, ikiwamo suala la usawa wa kijinsia ulimwenguni kote, kumekuwa na juhudi kubwa za kufanikisha juhudi za kumkomboa mwanamke kupitia vipindi, makala na matangazo kwenye redio, televisheni, kazi za fasihi, tovuti, blogu, magazeti, majarida miongoni mwa vyombo vingine (Wood, 2013). Msisitizo hasa umewekwa kwenye mtindo wa elimu-burudani *(Edutainment/Educational-Entertainment/ Information-Entertainment)* kwenye vyombo hivi (Wood, 2013). Elimu-burudani ni dhana iliyofumwa kuelimisha, kubadilisha mitazamo na mielekeo kupitia burudani. Imetumiwa na taasisi, mashirika, waandishi na vyombo vya habari kupitisha ujumbe wa kubadilisha maoni na mitazamo kuhusu masuala ya kijamii kama vile kupanga uzazi, magonjwa sugu na mazingira.

**1.2 Fasihi na Utetezi wa Mwanamke**

Fasihi ni njia au harakati mojawapo ambayo imetumiwa na inazidi kutumiwa kuhamasisha harakati za ukombozi wa mwanamke. Kwa miaka mingi, fasihi ya Kiafrika imekuwa ikimsawiri mwanamke kama kiumbe dhaifu aliyenaswa kwenye utata wa tandabui na kufungwa mikatale ya taasubi za kiume (Nyariki, 2014). Matokeo ya mitazamo hiyo hasi yakawa ni kumtengea mwanamke mazingira ya jikoni, kumwelemeza mzigo wa kuzaa na kulea, kumhini elimu ambayo ni mwangaza wa maisha na kumnyima nafasi ya usemi katika vikao vya 'mabwana' eti mwanamke ni 'kitwana'; yupo kuonekana wala si kusikika. Kama anavyosema S.A. Mohammed kupitia kipaza sauti chake, Kazija, katika riwaya ya *Utengano*: '…mwanamke (ni) mtumwa…viumbe vya kupika na kupakua, kufua na kupiga pasi, kushika mimba na kuzaa, kuzaa, kuzaa, kuzaa kama panya…'. Usawiri wa namna hii umeendeleza juhudi za kudumaza maendeleo ya mtoto wa kike katika bara la Afrika kwani anaelekea kukubaliana na nafasi aliyotengewa katika jamii.

Hata hivyo, wapo waandishi wachache wa fasihi ya Kiswahili ambao wamemsawiri mwanamke kwa namna tofauti, kwa mtazamo chanya. Tofauti na waliomsawiri mwanamke kwa mtazamo wa kijadi, mwanamke mtawa,

wanafasihi wa kundi la pili wanamsawiri mwanamke kisasa kwa mitazamo chanya. Wanafasihi hawa ambao sasa wanaegemea mtazamo-kike, wameona umuhimu wa kuwasawiri wahusika wa kike wanaoweza kuigwa na umma wa kike (Momanyi, 2002; Nyariki, 2014). Mathalani, Momanyi (2002) anaelezea uhusika wa Nakuruto kama mwanamke wa kisasa ambaye ni hamasisho la jamii kuhusu mengi yanayoikumba yakiwamo matatizo yanayotokana na uharibifu wa mazingira. Waandishi hao wa fasihi pia, wameonesha juhudi za mtoto huyo wa kike wa kisasa kujitanzua kutokana na kasumba za jamii na ubabe-dume. Katika makala haya, tunaonensha jinsi Mwalimu Andrew katika insha zake za kifasihi za mienendo za kila Jumapili kwenye gazeti la *Sunday Nation* (Kenya) na *The Citizen* (Tanzania) na *Daily Monitor* (Uganda) alivyofaulu kuchora taswira chanya ya mwanamke wa kisasa kwa kumwonesha kama mja aliyeelimika, akazinduka, akapata ujasiri, akawa na msimamo thabiti na kujitolea kuubirua nje-ndani mfumo wa kibabe-dume unaomnyanyasa na kumdhalilisha. Insha za mienendo hujishughulisha na kusawiri mienendo, mitindo na itikadi kwa kusudi la kuitanabahisha jamii kuhusu, athari za suala au mienendo hiyo kwa mielekeo na mitazamo ya jamii husika.

## 2.0 Sababu za Kuteua mada hii

Kiini cha mjadala wa makala haya kimetokana na tajiriba ya mwandishi akiwa kama mwanafunzi na mwalimu wa somo la fasihi. Kwa mfano, katika mihadhara na mijadala na wanafunzi wa chuo kikuu katika kozi za Nathari ya Kiswahili na Sanaa ya Maonyesho, kulizuka ubishi kuhusu kuaminika au kutoaminika kwa wahusika majagina wa kike katika kazi za nathari ya Kiswahili mintarafu ya ulimwengu wa karne ya 21. Ubishi ulielekea kuonesha kwamba mitazamo na kalautala waliyonayo wanafunzi kuhusu nafasi ya mwanamke wa kisasa katika jamii inawakilishwa na wahusika wa kike katika kazi hizi za nathari na za sanaa za maonyesho kwenye televisheni. Mathalani, Charity katika kipindi cha "Mother-In-law" kwenye Citizen TV na Fiolina kwenye makala ya *Staffroom Diary*, Sunday Nation kila Jumapili. Isitoshe, hivi karibuni waandishi wengi wa fasihi ya Kiswahili wamejikusuru kuandika kazi ambazo zinamchora mwanamke kama kiumbe mwenye nafasi yake na anayeweza kutumia nafasi hii kujitetea katika jamii (Nyariki, 2014). Azma ya uchunguzi huu ilikuwa kutafuta ushahidi wa kijarabati katika kuthibitisha uhalali wa madai haya.

Kwa kutumia makala teule ya insha za *Staffroom Diary,* utafiti ulinuia kubainisha usawiri chanya wa mwanamke wa kisasa katika makala haya ambayo

huandikwa kwa mseto wa Kiswahili na Kiingereza na kujadili athari za usawiri huo kwa hadhira ya wasomaji. Hadhira iliyotumika katika makala haya ni wanafunzi ambao ni wasomaji wa makala haya.

## 3.0 Kiunzi cha Nadharia

Katika kutekeleza azma ya makala haya, mwandishi ametumia Nadharia ya Upalizi. Hii ni nadharia inayotathmini matokeo ya vyombo vya habari kwenye mitazamo ya hadhira yake. Nadharia hii ambayo ni ya uanahabari, inaeleza kwamba jinsi watu wanavyozidi kutagusana na makala na vipindi kwenye vyombo vya habari, ndivyo wanavyokuja kuamini kuwa uhalisia katika jamii unaoana na ule wa kwenye vyombo vya habari. Nadharia hii inapania kuhalalisha maoni kuwa vyombo vya habari ndivyo hufinyanga jamii na pia kwamba ingawa wakati mwingine yaliyomo kwenye vyombo hivi huwa si uhalisia; utazamaji, usikilizaji na usomaji wake aghalabu, hatimaye huja kupalilia na kujenga mtazamo kuwa hayo ndiyo kiwakilishi cha picha halisi ya jamii (McQuail, 1987). Kwa muktadha huu, wanawake ambao wameoneshwa kwenye makala ya *Staffroom Diary* kama walioelimika, wanaotambua haki zao, wanaong'ang'ania nafasi za kiuchumi, kisiasa na kiutawala sawa na mwanamume ni kiwakilishi halisi cha mwanamke katika karne ya 21.

Watafiti kadhaa wameitumia nadharia hii katika uwanja wa fasihi na matokeo yake ya kijarabati yamedhihirisha ufanisi wa kiwango cha juu (Garbner na wenzake, 1977, 1978, 1979, 1980) na Okunna (1992, 1995). Kwa mujibu wa Shrun (1995), hadhira inapotagusana na usimulizi na maudhui yanayorudiwa mara kwa mara hutarajia mambo haya kuakisiwa katika maisha yao halisi.

Katika kushamirisha ukweli wa machukulio ya Nadharia ya Upalizi, Albert Bandura alipendekeza kiunzi cha Ujifunzaji Jamii na kusema kuwa imani, mitazamo, mielekeo, na kalautala za watu hutokana hasa na yale wanayoyaona, kusikia na kusoma katika vyombo vya habari kuliko tajiriba zao halisi maishani mwao (Bandura, 1977). Anazidi kusema kwamba, hadhira hujifunza tabia, mielekeo na mitazamo kwa kutazama na kuiga wahusika wa kibunifu kwenye kazi za sanaa. Hata katika tajiriba na hali halisi ya mambo; bado mitazamo yao huelekezwa tu na 'uhalisia' wa vyombo vya habari. Nadharia hii basi ni mwafaka kuchambua insha za kifasihi zinazochapishwa katika makala za magazeti kwa kuwa inasisitiza kuwa vyombo vya habari vina nafasi kubwa sana ya kuathiri taasubi za wanajamii.

## 4.0 Uwezo wa Vyombo vya Habari

Uwezo wa yaliyomo katika vyombo mbalimbali vya habari yakiwamo makala ya kifasihi zinazochapishwa magazetini, umezua mjadala ulimwenguni kote. Katika muktadha wa Afrika Mashariki, tumeshuhudia tuhuma nyingi kutoka kwa wahakiki wa fasihi kama vile Evan Mwangi, dhidi ya utanzu wa fasihi wa nyimbo za kizazi kipya (video na maneno yake) zinapotosha tabia za vijana, kudunisha wanawake na kuchafua utamaduni wa Mwafrika (Mwangi, 2009). Uchunguzi wa Jumanne (2016) kuhusu athari za unywaji pombe miongoni mwa vijana Tanzania unaonesha kuwa taswira zinazotukuza unywaji pombe kwenye magazeti na televisheni zimechochea na kukuza mtazamo miongoni mwa vijana kuwa ulevi ni hulka ya kujivunia. Nao Mlacha na Madumulla (1995) wanadahili kwamba wahakiki wengi wa fasihi wamedai kwamba riwaya pendwa za Ben Mtobwa kama vile, *Dar es Salaam Usiku* zinapotosha mtazamo wa vijana kuhusu uhuru na starehe. Maoni yote haya ya kitaalamu yanadhihirisha uwezo wa yaliyomo kwenye fasihi na vyombo vya habari: redio, televisheni, vitabu vya fasihi, majarida, magazeti, blogu na tovuti katika kuchochea ujenzi wa taswira na mitazamo miongoni mwa wanajamii.

## 5.0 Mbinu za Utafiti

Data katika utafiti huu ilitokana na vyanzo vikuu viwili ambavyo ni usomaji wa makala za magazeti husika pamoja na hojaji au majadiliano na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro nchini Kenya. Taarifa za makala haya zilitolewa na jumla ya watafitiwa 20 ambao ni wanafunzi wa mwaka wa tatu wa kozi ya Sanaa za Maonyesho ya Kiswahili waliochaguliwa kimakusudi. Kati ya hao, wanafunzi 14 walikuwa wa kike, na wanafunzi 6 walikuwa wa kiume. Kadhalika, insha 15 za makala za *Staffroom Diary* zilizoandikwa kati ya Novemba 29, 2015 na Machi 31, 2018 zilisomwa na kutumiwa katika mijadala yetu. Masuala ya kubainishwa yalitokana na vipengele vifuatavyo katika makala:

i. Jinsi wanawake walivyosawiriwa katika makala haya kupitia kwa wahusika wakuu wa kike (kwa njia chanya) na iwapo wanaaminika au hawaaminiki.
ii. Athari ya taswira hizi kwa mitazamo ya watafitiwa kuhusu wanawake.

## 5.1 Uchambuzi wa Data ya Utafiti kutoka Maktabani

Kama ilivyodokezwa, data ya msingi ya makala haya ilikusanywa kupitia mbinu ya usomaji na uchambuzi matini. Katika mbinu hii, makala mbali za insha zilizomo kwenye mkusanyiko wa makala ya *Staffroom Diary* zilizomwa na kuchambuliwa. Huu ni mkusanyiko wa insha za mienendo zinazoegemea upande wa elimu-burudani ambayo husaidia hadhira (wasomaji) kujifunza mienendo inayokubalika katika jamii kwa njia chanya kutoka kwa wahusika wa sanaa hii. Makala haya yalianza kuchapishwa mwaka 2009. Ni masimulizi ya kitashtiti kuhusu maisha ya mhusika aitwaye mwalimu Andrew maarufu kwa jina la 'Dre' ambaye ni mhusika mkuu. Dre pia anasomea digrii ya ualimu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, hali inayomwezesha kuzungumzia masuala ya mjini na shambani kwa uketo. Masimulizi yanazungukia mwalimu Dre na mkewe, Fiolina, jumuia ya shule ya Msingi ya Mwisho wa Lami; Mwalimu Mkuu, Skastina Majani maarufu kwa jiana la 'Bensouda'; walimu wa kike: Madam Nzomo, Madam Mary, Madam Anita, Mrs. Atika, Madam Ruth, Madam Sella, Madam Lena na walimu wa kiume: Kuya, Oscar, Saphire, Lutta, Oscar na Eric. Makala huandikwa kwa mtindo wa uchanganyaji msimbo wa Kiswahili na Kiingereza. Mhariri wake, Martin Mwangi anasema kwa kuchanganya msimbo, mtunzi hufanikisha matumizi ya 'lugha ya mwananchi' ambayo hufikia na kuvutia hadhira pana (Khalayi, 2015). Kutokana na ufundi wake, insha hizo zimewavutia wasomaji wa makundi na marika mbalimbali na hatimaye kuathiri mitazamo ya wasomaji wake. Utafiti huu ulidhamiria kubainisha mambo mawili: (i) kuonesha usawiri chanya wa wahusika wa kike na (ii) kujadili athari za usawiri huo kwa wasomaji wake.

Masuala yanayohusu usawiri chanya wa wanawake yamejitokeza katika insha mbalimbali za makala teule maarufu kama *Staffroom Diary*. Katika makala ya Desemba 20, 2015, "*Fiolina Leaves me over Magufuli-style Austerity*," Fiolina anamwacha Dre kwa kutohusishwa katika uamuzi wa kupunguza gharama ya matumizi ya nyumbani mwao. Dre amepunguza gharama ya chakula, urembo wa Fiolina, na masurufu. Kwa mujibu wa Kipyegon (2013),, maamuzi ya familia, jamii na maisha kwa ujumla ni shughuli za mwanamume. Ingawa mwanamke huwa na mchango muhimu katika maamuzi ya masuala ya kijamii, aghalabu hashirikishwi lakini hulazimika kuitikia maamuzi ya mwanamume. Fiolina anabirua mfumo huu kwa kuhama ndoa hii na kurudi kwao hususani anapogundua kuwa Dre anazidi kusisitiza msimamo wake na kushika kani kuwa halegezi kamba.

Suala la usawiri chanya wa taasubi za wanawake pia linaelezwa katika makala, "It is better to walk away than put up with a violent man" Saturday Nation, Julai 1, 2017. Katika makala hiyo, tunaelezwa habari za Njoki Kaigai maarufu kwa jina la '*City Girl*'. Inaeleweka kuwa wanawake wengi huvumilia ndoa ambazo huwanyanyasa na uamuzi wao hautambuliwi. Mwanamke amenyimwa uwezo wa kukataa maelezo na maelekezo yoyote anayoambiwa na mumewe hata kama anayoambiwa yanaathiri maisha na ndoa yake. Mwishowe wengi wao huvumilia wakiumia kihali na mali. Anasema uvumilivu si suluhu. Kama mazungumzo, mashauriano na ushawishi havizai matunda, lugha inayoweza kusikika kwa mfumodume kama huu ni kuhama ndoa badala ya kuamua kupigana na mwanamume; kwani apigaye ukuta huumiza mkonowe. Uhalali wa mtazamo huu unadhihirika Dre anapolegeza msimamo baadaye na Fiolina anarejea.

Katika makala ya Septemba 23, 2016, *"My inability to complete degree and house leaves Fiolina fuming,"* Dre anapozomewa na kukosolewa na Fiolina kuhusu uraibu wake wa pombe unaohujumu uwezo wa kukamilisha ujenzi wa nyumba yao na kumaliza kusomea digrii ya ualimu. Dre anaazimia kumzaba kofi. Kwa ukakamavu, Fiolina anamkabili kwa maneno yenye msimamo thabiti, *"Unataka kunipiga? Unataka kunipiga Dre? Siwezi kukaa hapa."* Anafungasha virago na kuondoka. Mbinu hii inaonekana kufua dafu aghalabu, kwani Dre hunyenyekea baadaye na kubadili mienendo. Fiolina anarejea hatimaye. Mwandishi anamchora mwanamke wa kisasa kama mhusika anayeonesha ujasiri katika kupambana na changamoto ambazo zinamkabili. Ripoti ya uchunguzi ya *World Economic Forum (Global Gender Gap Report, 2016)* inatambua haja ya kuwashirikisha wanawake katika maamuzi mbalimbali ya kijamii. Inaaminiwa kuwa hatua hii itachangia katika kujenga na kufikia malengo ya usawa, maendeleo na amani kwa wote.

Asasi za ndoa na elimu pia zinasaidia kuendeleza mfumo wa kibabedume kwa kumfanya mwanamke kuwa mtumwa wa mwanamume. Mwanamke analazimika kumtegemea mwanamume kiuchumi na hapewi nafasi yoyote ya kumshauri mume wala kuchangia katika kujiinua kiuchumi (Beauvoir, 1988). Hali hii inafanikishwa kwa kuhakikisha kwamba mwanamke hapewi elimu na akipewa, kiwango chake ni cha chini kuliko apewayo mwanamume. Dre anaona karo anayomlipia Fiolina Mosoriot TTC anaisoza. Anauza ng'ombe wake kujilipia karo yake mwenyewe ila siyo Fiolina. Anasema, "…Kufanya hivyo ni kama kuuza ng'ombe kumpeleka ng'ombe mwingine shuleni" (makala ya Januari 3, 2016, *"These are my resolutions for 2016, so help me God")*.

Hata hivyo, wanawake wa kisasa wamejikusuru kupata elimu na kubadilisha hali hii. Muniu (2013) anasema kuwa wanawake walioelimika huweza kutambua haki zao na kuzidai ilhali baadhi ya wanawake ambao hawakufanikiwa kupata elimu hushindwa kutambua haki hizo. Wanawake katika makala haya wanaipitua hali hii kwa kuenda shuleni na kutambua haki zao. Dre anasema, *"…wanawake waliosoma kama Fiolina…wanaweza kukusimamia, kukusubukua, kukusuta na hata kukukaidi."* (Aprili 23, 2017, *"Hard time feeding these mouths").* Wanawake wengi wamegundua umuhimu wa elimu na sasa wameenda shuleni. Miongoni mwa walimu wa Shule ya Msingi ya Mwisho wa Lami, wanane ni wanawake na watano ni wanaume. Hata katika shule ya kibinafsi ya Sharp Shooters Academy ambako Fiolina anafundisha, Dre anasema, "…nilishtuka kugundua kuwa wengi wao (walimu) ni wanawake" (makala ya Mei 7, 2017, "I am moving in with Fiolina").

Usimamizi wa taasisi za kazi umetwaliwa na wanawake. Ukweli ni kwamba nafasi ambazo zilipaswa kuchukuliwa na wanaume siku hizi zinajazwa na wanawake. Hali hii inatishia ubabe wa mwanamume. Mathalani, usimamizi wa shule ya Mwisho wa Lami unabadilishwa kati ya walimu wakuu wa kike tu. Bensouda anaposimamishwa kazi, Catherine anapewa cheo hiki. Baadaye Bensouda anarejeshewa mamlaka hayo (*"Bensouda's return dims my hope to be principal" Sunday Nation*, Januari 28, 2018).

Wanaume wanaposhindwa kupata madaraka kwa vile hawana sifa na mahitaji ya kutosheleza cheo hicho, wanabaki kujisifu kuonesha kiwango chao cha elimu, anavyofanya Dre. Anasema yeye amesoma kuliko Bensouda na hivyo anafaa kuwa mwalimu mkuu. Wivu unapozidi wanaamua kutumia nguvu kuwaondoa wanawake mamlakani. Dre anapanga na wanakijiji kuandamana ili kumwondoa Bensouda lakini anagonga mwamba *("Cracks in Mwisho wa Lami gave me hope of replacing Bensouda" Sunday Nation*, Machi 18, 2018).

Elimu imemzindua mwanamke wa kisasa kuweza kushiriki shughuli aghalabu zote zinazomhusu yeye, jamii na familia yake. Wanaume wanawaogopa wanawake waliosoma. Hawa ni wale ambao hukalia wanaume (Millet, 1977). Hitler, muuzaji wa pombe haramu anayoipenda Dre, anamuusia hivi Dre, "Kuoa mtu aliyesoma ni kitu mzuri…chunga asikukalie" (makala ya Agosti 27, 2016, *"I borrowed cash from my wife and became a laughing stock."* Dre anasema tabia za Fiolina baada ya kukamilisha masomo ya chuo cha walimu wa shule za msingi cha Mosoriot ni tofauti na alivyokuwa kabla ya kuelimika. Sasa hivi anatambua haki zake na kushiriki uamuzi wa kifamilia. Katika makala ya Agosti 14, 2016, *"Fiolina pestering*

*me to top up loan to complete house*", Dre anasema, "Fiolina ambaye Mosoriot TTC imenirejeshea ni tofauti na yule wa awali…amekuwa mkakamavu na jasiri anayetoa uamuzi nyumbani na kusisitiza uzingatiwe. Uamuzi wangu siku hizi umebaki kuwa mapendekezo tu…awali mapendekezo yangu yalikuwa ndio uamuzi." Anasema hivi kuhusu ukakamavu wake, "…siku hizi Fiolina ananiita huku akiniangalia usoni moja kwa moja." Mwanamke wa kisasa hanyamazi na kuumia kimya kimya iwapo hali inamkalifu na kumdhulumu kama mwanamke wa awali (Momanyi, 1998). Mathalani, Fiolina anamfukuza Dre kutoka katika chumba chao cha malazi kwa sababu ya ulevi unaomfanya kushindwa kutekeleza majukumu ya kindoa. Vilevile, Fiolina ameshindwa kustahimili harufu ya pombe na hivyo anachukua hatua ya kujirejeshea amani na utulivu *("Why I am not about to buy Fiolina any of the strange food" Sunday Nation*, Machi 31, 2018).

Mwanamke anamshinikiza mwanamume kuchukua hatua ya kujiimarisha. Dre anapolalamika hana pesa za kumaliza kujenga nyumba, Fiolina anamliwaza, "*So what?* Tutaishi hivi?... pesa hutafutwa boss!" Fiolina anatumia silaha ya mwisho anayoiamini ya kuhujuru ndoa kumshinikiza Dre achukue hatua ya kutimiza malengo ya familia; kumaliza kusomea digrii na kumaliza kujenga nyumba yao. Tazama, *"My inability to complete degree and house leaves Fiolina fuming" Sunday Nation***,** Septemba 23, 2016.

Kikwazo kingine kinachokabili ufanisi wa harakati za kujenga usawa wa kijinsia ni uwezo duni wa mwanamke kiuchumi (Muniu, 2013). Katika makala zilizochambuliwa imeoneshwa ni kwa jinsi gani mwanamke wa kisasa amekuwa mwanajamii anayejiweza na kujitegemea anayeweza kudai haki yake. Hii ni kwa sababu mhitaji hana chaguo isipokuwa kuitikia matakwa ya mfadhili wake ilivyo na kwamba aghalabu wanawake wengi huwa hawajiwezi kiuchumi. Kwa sababu wanaume wanaelewa udhaifu huu wa wanawake, wanajihifadhia hadhi kwa kuwapa wanawake masharti fulani. Mwanamume hujaribu kumfanya mwanamke akose kupata kazi au kutengeneza pesa zake mwenyewe (Beauvoir, 1988). Humfanya amwitishe pesa zozote anazohitaji. Au anaweza kumlazimisha kufanya kazi, amwekee masharti ya kazi kisha achukue mapato yake. Katika makala ya Septemba 25, 2016, *"Fiolina rejects my new rules of engagement to save our marriage",* haya yanadhihirika. Dre anajaribu kudhibiti uhuru wa Fiolina shuleni wanakofundisha wote. Mtafaruku unapozuka Fiolina anapokaidi kanuni hizo, ushauri anaopata ni wa kihafidhina. Alphayo anamrai hivi, *"Vijana wa siku hizi you have jokes… why do you want your wife to work like you?... kwanza wewe Andrea na mshahara*

*kubwa wacha bibi akae nyumbani.*" Rasto anasema, *"Makosa sio Fionila kufanya kazi…Makosa ni kufanya kazi ofisi moja na Andrea…Mwanaume anafaa kukuwa na siri. Utakuwaje na siri kama mnaenda ofisi moja na bibi kila siku?"* Kulingana na Pilcher na Imelda (2004), Wafeminsti wanashuku kuwa uhafidhina ni pingamizi katika uletaji wa usawa wa kijinsia katika jamii. Wanalaumu hali ya kutamani tofauti za kiwajibu kulingana na jinsia katika jamii. Aghalabu, wanawake kwa wanaume wangependa kuwe na mpaka bayana wa kiwajibu kulingana na jinsia. Kwa kuzingatia mtazamo huu, nafasi ya mwanamke huchukuliwa kuwa jikoni na ulezi wa watoto.

Wanawake wameamua kujiinua kielimu na hivyo kiuchumi wanapopata kazi na kukiuka vikwazo wanavyowekewa na wanaume. Dre anapodhamiria kumwachisha Fiolina kazi Sharp Shooters Academy kwa kutolipwa mapema, Fiolina anamshambulia, "Ni wewe uliyefanya mahojiano ya kazi au mimi?" Anapomuuliza kima cha mshahara alichoahidiwa kulipwa, anamuuliza Dre, "… Umewahi kuniambia kima cha mshahara wako?... kwa nini nikwambie wangu?"

Aghalabu jamii nyingi hasa za Kiafrika humtarajia mwanamume kushughulikia masuala ya ulinzi, uongozi, mamlaka na maamuzi na mwanamke. Hata hivyo, wanawake wa kisasa wameupindua mfumo huu, wameshika usukani na kuonekena vielelezo vya ufanisi wa kiuchumi na uongozi katika jamii. Hoyt (2010) anasherehesha kuwa wanawake huendesha taasisi kama walezi ilhali wanaume huziendesha kama wasimamizi. Hii imesababisha wanawake kuibuka kama viongozi bora, suala linalozidi kuwaogofya wanaume na hivyo wanazidisha juhudi za kuwakwaza wanawake. Wanajaribu kutambulisha ufanisi wa taasisi na juhudi za wafanyakazi wa kiume tu katika taasisi hizo hata kama viongozi ni wanawake. Katika makala ya Januari 1, 2016, *"I love Mwisho wa Lami, but now I must leave"*, Dre amehamishiwa shule jirani. Wazazi wa kiume wanaona kuwa shule ya Mwisho wa Lami itadidimia kwa kuondoka kwake. Lutta anasema, "Bila wewe (Dre) Bensouda (Skastina Majani - mwalimu mkuu wa kike) atatuharibia watoto wetu." Wanachukulia kuwa matokeo mazuri katika shule hiyo yametokana na mchango mkubwa mwanamume (Dre), ambaye ni naibu wa mwalimu mkuu ila sio kazi ya mwanamke, Bensouda. Hii ni licha ya kuwa tangu ujio wa Skastina matokeo ya Mwisho wa Lami yameimarika ("Why Bensouda is the best HM" *Sunday Nation*, Machi 27, 2016).

Wanawake ni wachapakazi na watimiza malengo. Kutokana na sifa hizi wanaishia kupewa lakabu ambazo ni taswira za msimamo thabiti. Skastina Majani

anarejelewa kama 'Bensouda' kutokana na jina la mwendesha mashtaka wa korti ya ICC wakati wa kesi za jinai zilizowakabili viongozi wa Kenya kufuatia vurugu za baada ya uchaguzi wa mwaka 2007. Kutokana na ushurutishi na kutotikisika kwake Skastina kimsimamo, anapewa lakabu hii 'Bensouda'. Mbali na hilo Dre na jamii inamrejelea Skastina kama "Female Headmaster" (Mkuu wa shule mwanamke). Neno 'headmaster' kwa wengi linazua taswira ya kiongozi mkali, asiyetetereka. Viongozi wa kike wawili Skastina na Prof. Olive Mugenda, aliyekuwa Naibu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kenyatta (anakosomea digrii, Dre) wanarejelewa kwa lakabu ya 'Headmaster'. Anamwita Prof. Mugenda "University Headmaster". "Headmaster" ni kiwakilishi cha "mamlaka". *("These are my new resolutions for 2016, so help me God", Sunday Nation*, Januari 03, 2016).

Isitoshe, wanawake wanaonekana kama kilele cha ufanisi kiuchumi. Licha ya kuchukulia kuwa mwanamke hawezi kufanikiwa bila mwanamume, Dre anashtuka anapogundua kuwa Bensouda alinunua gari mwenyewe. Licha ya kuwa ni mwanamke, ndiye wa kwanza kumiliki gari mbali na watu wanaoishi Nairobi kama vile Pius, kakake Dre. Magari mengineyo kijijini huwa ya serikali hasa Maafisa Wadhibiti Ubora wa Elimu na Viwango. Dre anasema, "Sikudhani linaweza kuwa lake (gari)…lazima ana bwana tajiri mjini…" *("History made as our school gets first car", Sunday Nation,* Septemba 04, 2016).

Wanawake pia wanaonekana kupigania nafasi zao wanapokabiliwa na tuhuma zinazotishia kuwaondoa madarakani. Bensouda anaposimamishwa kazi kwa tuhuma za ufisadi. Anatoa tahadhari kuwa hataondolewa kwa urahisi na kuonya mahasidi na watuhumu wake, "Mwalimu Kuya, waambie wale wafadhili wako kuwa sitakufa kikondoo na kuwatazama wakiingilia masuala ya shule…waambie wachunge sana" *("Bensouda on the warpath after protests against her"* Juni 05, 2016). Anapoondoka, anakita kambi katika Ofisi za Tume ya Kuajiri Walimu (TSC) Nairobi kupigania haki zake. Anaporejeshwa kazini anamwambia Dre, "Usicheze na mimi, nina mbinu na ninajua haki zangu…" *("Bensouda is back, poor me"* Juni 03, 2016)

Mbiti (1969), anaeleza kuwa katika jamii za Kiafrika kuna imani kuwa raha ya ndoa ni kupatikana kwa watoto. Aidha, ndoa yenyewe hutambulika pale tu mwanamke atakaposhika mimba na kuzaa. Mwanamke anaposhindwa kuzaa watoto hata kama atakuwa na sifa nyingine nzuri, nyumba hiyo hujawa na huzuni na hujiona kama wana mkosi na laana kutoka kwa wahenga wao. Pia, mwanamke anapokosa uzazi huaminika kuwa ametenda kosa kubwa sana. Kutokana

wa mtazamo wa jamii ya Kiafrika, watu wanapooana lazima wazae. Lakini mwanamke ndiye huonekana kiini au mlengwa wa kuleta matunda. Kunapotokea matatizo ya uzazi katika familia, mtu wa kwanza kulaumiwa ni mwanamke na siyo mwanamume. Mwanamke huanza kupata manyanyaso kutoka kwa familia, jamaa na marafiki. Katika *"Pregnancy crisis looms in school"*, Juni 03, 2017 walimu wa kike sita ni wajawazito. Bensouda anamwuliza Dre kwa nini Fiolina hajapata himila. "Na wewe, kitu gani kinaendelea kwako? Miaka mitano sasa na hakuna matokeo… kuna shida? Tunaweza kusaidia." Suala hili halimfadhaishi Dre. wala Fiolina. Wote wawili wanaelekea kutambua kuwa kuzaa ni majaliwa ya Mwenyezi Mungu na hali hii husababisha kusambaratika kwa ndoa nyingi hasa kutokana na shinikizo kutoka kwa wazazi na ndugu, jamaa na marafiki wengine lisiposhughulikiwa kwa uangalifu.

### 5.2 Maoni na Mtazamo wa Hadhira ya Wasomaji

Watafitiwa walikuwa wanafunzi 20 wa umri kati ya miaka 20 na 25. Watano (25%) walikuwa na miaka 20. Wote hawa walikuwa wasichana waliokamilisha elimu ya kidato cha nne wakiwa na umri wa miaka 17. Wawili (10%) walikuwa na umri wa miaka 25. Mmoja alikuwa wa kike, mwingine wa kiume. Wanafunzi wawili walieleza kuwa walikatiza masomo wakiwa mwaka wa pili kwa sababu za ukosefu wa karo, kisha kurejea baada ya miaka minne. Walijiunga na chuo mwaka wa 2010 wakaacha mwaka wa 2012 na kurejea tena mwaka 2016, Septemba. Waliobaki kumi na watatu (65%) walikuwa na umri wa miaka 22. Watafitiwa 6 (30%) walikuwa wa kiume.

Watafitiwa wote 20 walikiri kuwa wafuasi wa makala ya *Staffroom Diary,* wakiyafuatilia wiki baada ya wiki kwenye magazeti au kwenye mtandao tangu walipomaliza kidato cha nne. Watafitiwa kumi na wanane (90%) walikiri kuwa nafasi ambayo mwanamke amepewa katika makala haya ni chanya, hasa wakitaja wahusika wakuu wawili wa kike: Fiolina na Skastina Majani (Bensouda). Katika makala haya, wanasawiriwa kama wanawake wa kisasa wasiotishwa na mfumodume. Wamezinduliwa na kuwezeshwa na elimu na wako tayari kumenyana na wanaume kukomboa hadhi yao katika jamii hasa katika asasi ya ndoa na uongozi. Akizungumzia usawiri wa mwanamke katika makala haya, Khalayi (2015:81), anasema:

Ni mwanamke wa kisasa aliyeenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Humenyana na wanawake kwa wanaume na kubuka mshindi masomoni si mara

chache…akataka kufanya kazi za kibega, akazifanya akafanikiwa. Almuradi siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume…hakuna kazi isiyofanywa na mwanamke siku hizi (Tafsiri yangu).

Ni muhimu kwa wahusika kuaminika na kukubalika kupitia lugha na vitendo vyao. Wahusika hawa wanaoaminika na kukubalika huwakilisha watu wa kawaida katika jamii. Hao huitwa wahusika mviringo (Stacy, 1997). Walipoulizwa kuhusu uaminikaji wa nafasi ya mwanamke katika makala, kumi na wanane (90%) walisema kuwa wahusika wa kike, majukumu yao yanaaminika na yanawezekana katika hali halisi. Khalayi (2015) anasema kuwa mwandishi wa makala haya amefaulu kuaminisha wahusika wa kike na matukio katika kazi yake kupitia majina ya wahusika, kazi zao, mandhari, lugha na matendo yao. Matumizi mazuri ya uhusika yanafanya wasomaji na au hadhira yake kujihusisha na kujitambulisha na visa au matukio katika masimulizi yake. Kuhusu iwapo wanaweza kumtambua mwanamke yeyote katika maisha yao halisi anayeafiki sifa za wahusika wakuu wa kike wote kumi na wanane (100%) walikubali kuwa wapo. Kwa ujumla, wachache (10%) walisema makala haya yanapotosha kuhusu nafasi ya mwanamke kwa kumwonesha kama mdaku, mwenye kidomo na mkware wakirejelea makala ya Novemba 29, 2015, *"Drama as Apostle goes with Nyayo's wife to meet Pope"* inaposemekana Anindo, mkewe Rasto alikimbia na Mhubiri Elkana kwenda kula uroda.

Kuhusu uwezekano wa makala haya kuathiri jamii na kuifanya ijenge kalautala kuhusu wanawake na uhalisia wa kijamii, wengi walikubali kuwa yana uwezo mkubwa wa kubadilisha mtazamo na mkabala wa jamii kuhusu wanawake na masuala yanayowahusu. Wengi walisema kuwa walikuwa wameshaathiriwa na makala haya kwa njia chanya na kuwafanya wajenge kasumba kuwa hali, sifa na hulka za wahusika wake wa kike ndio uhalisia wa mwanamke wa kisasa.

Vigeu vya umri na jinsia pia ni muhimu katika utafiti huu. Watafitiwa wote wa kike isipokuwa (33%) ya wa kiume walikubali kuwa usawiri wa wanawake katika makala zilizochunguzwa ni uhalisia katika jamii, wanajitambulisha na wahusika hawa na wangeweza kutambua wanawake wenye hali, sifa na hulka hizi katika jamii. Wahusika wote wa umri wa miaka 22 na zaidi walikubali kuwa makala haya yana uwezo wa kuathiri na kubadilisha mitazamo katika jamii kuhusu wanawake na nafasi yao katika jamii.

## 6.0 Matokeo ya Utafiti na Mapendekezo

Uchambuzi wetu unaonesha kuwa makala haya yamesaidia kuonesha usawiri halisi wa nafasi chanya ya mwanamke wa kisasa. kwa kufanya hivyo, makala pia yamefanikiwa kufikia lengo la karne ya 21 ambapo kuna jitihada nyingi zinafanywa ili kumwezesha mwanamke kiuchumi, kisiasa na kijamii. Taswira za mwanamke aliyeelezwa katika makala hizo zinaaksi muktadha wa mwanamke wa kisasa aliyekulia katika mazingira yaliyobadilika. Hivyo, hata matarajio yake maishani ni tofauti kabisa na yale ya wanawake walioishi mapote mawili yaliyopita; wanawake makamu ya nyanyake na mamake-kuu.

Katika makala yaliyochunguzwa kupitia wahusika wakuu wa kike, mwandishi amefanikiwa kuonesha kuwa mwanamke wa kisasa ni kiumbe asiyekubali kuteswa kisha akafyata ulimi. Anapokandamizwa, naye hupigania haki yake kwa dhati na hamasa. Kamwe hakubali 'mahali pake' katika jamii alipotengewa na wanaume wenye mawazo ya kihafidhina yaliyopitwa na wakati. Halikadhalika, haamuliwi katika jambo lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Anashiriki kutoa mwelekeo kuhusu masuala yanayomwathiri yeye, maisha yake na ndoa yake. Amegeuza mfumo uliomdhalilisha hapo awali na kuvitumia vigezo vilivyotumiwa kumkandamiza kama vile mimba na talaka kumfaidi na kumsaidia kupaza sauti yake na kusikika.

Utafiti umeonyesha kuwa magazeti ni wenzo muhimu katika kueneza, kubadilisha na kuimarisha mitazamo, maoni na mielekeo ya umma. Kutokana na uamilifu wake wa kuarifu, kufunza na kuburudisha, magazeti yamepokelewa kwa wazi miongoni mwa watu wazima na watoto na matabaka mbalimbali kutokana na kuwa kila kikundi cha jamii kinashughulikiwa katika magazeti haya. Magazeti ya *Daily Nation, The Citizen na Daily Monitor* huweza kuifikia hadhira kubwa wakiwamo wanafunzi wa viwango mbalimbali vya elimu ambao ni wapenzi wa makala ya *Staffroom Diary*. Hivyo, wahariri na waandishi wa makala magazetini wanahimizwa kutilia maanani uwezo wa makala magazetini kukuza au kudunisha nafasi ya mwanamke katika jamii na mwishowe kujenga kalautala kwa hadhira yake.

Aidha, kuna haja ya waandishi wa kike kujibwaga katika uandishi wa fasihi ya Kiswahili. Walibora (2017) anabainisha uchache wa waandishi wa fasihi wa kike wanaodiriki kuandika kwa Kiswahili. Wananadharia na wahakiki wa mtazamo-kike wanapendekeza wanawake kuzamia uandishi wa kazi za kifasihi ambazo zinalenga matumizi ya lugha ya kike yenye usanifu mzuri na zinazohusu tajiriba ya wanawake (Momanyi, 2002). Hii itawahimiza wanawake kujitambulisha na

waandishi wa jinsia yao na wahusika katika kazi zao. Hatimaye, watawaiga na hivyo kushiriki wenyewe katika kujikomboa dhidi ya hali dhalilishi za mfumodume.

Wafuasi wa Nadharia ya Ufeministi wanapendekeza fasihi itumiwe kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu, hali aliyomo mwanamke ili kumsaidia mtu yeyote kuielewa hali hiyo (Wafula na Njogu, 2007). Wanaitifaki wenyewe wanapendekeza kwamba wahusika wanaosawiriwa katika kazi za fasihi wawe wanaostahili kuigwa kimienendo na kitabia. Mintarafu maoni haya, ni bayana kuwa mwandishi wa makala ya *Staffroom Diary* amefaulu kumwonesha mwanamke wa kisasa na utambulisho wake kamili na halisi katika jamii kwenye insha zake zilizochunguzwa.

## 7.0 Hitimisho

Makala haya yalinuia kutathmini usawiri wa mwanamke katika makala ya *Staffroom Diary* pamoja na kujadili athari ya usawiri huo kwa hadhira ya wanafunzi wanaosoma insha za makala husika. Imegunduliwa kuwa makala na insha zilizochunguzwa zina ufuasi mkubwa wa usomaji na mwanamke amesawiriwa kwa njia chanya za namna mbalimbali. Kadhalika, mwandishi wa makala haya amebaini kuwa makala yaliyochunguzwa yana uwezo wa kubadilisha mtazamo wa hadhira kuhusu wanawake. Hii inatokana na mwitiko mkubwa wa watafitiwa kuwa jinsi ambavyo mwandishi amemsawiri mwanamke, inaafikiana na hali halisi. Makala yanamwezesha mwanamke kujiamini na kupunguza kasumba hasi kuhusu wanawake katika jamii za kimfumodume.

## Marejeleo


De Beuvoir, S. (1994). The Second Sex. Chapa ya Picador Classics (1988) London: Pan Books

Bandura, A. (1977). Social Learning Theory. New York: General Learning Press.

Engels, F. (1884). The Origin of Family, Private Property and the State. New York: Cosimo Inc.

Gabner, G. (1979). "Demonstration of Power. Violence Profile No. 10". *Journal of Communication*. Summer, uk. 177-196

Gabner, G. (1978). "Cultural Indicators: Violence Profile No 9". *Journal of Communication*. Summer uk. 176-207

Gabner, G. (1977). "TV Violence Profile No. 8: The Highlights". Journal of Communication. Spring uk. 171-180

Gabner, G. (1969). Toward "Cultural Indicators": The Analysis of Mass Mediated Public Message Systems. *AV Communication Review* III Vol. 17

Gallagher, M. (1995). "Communication and Human Dignity: Women's Rights Perspective". *Media Development.* Vol. XIII, uk. 6-9

Global Gender Gap Report 2016. http://reports.weforum.org/global-gender-gap-report-2016/results- and-analysis

Hoyt, C. (2010). Women, Men and Leadership: Exploring the Gender Gap at the Top. *Social and Personality Psychology Compass.* University of Richmond: Blackwell Publishing Limited.

Jumanne, H. (2016). Wataalamu: Tanzania Iwe na Sera Maalum Kudhibiti Matumizi ya Pombe. *Mwananchi News*, Dar-es-Salaam: Mwananchinews.co.tz. Toleo la 16.05.2016.

Khalayi, R. (2015). "The Use of Humour in Socio-political Commentary in Mwalimu Andrew's 'Staffroom

Diary'. M.A. Thesis, University of Nairobi.

Kipyegon, K. (2013). "Nafasi na Utambulisho wa Mwanamke Katika Natala na Kifo Kisimani". Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mlacha, S. na Madumulla, J. (1995). Riwaya ya Kiswahili. Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam University Press.

McQuail, D. (1987). Mass Communication Theory: An Introduction (Second Edition). London: Sage.

Millet, K. (1970). Sexual Politics. London: Virago Press.

Momanyi, C. (2002). Suala la Uana Katika Fasihi ya Kiswahili". Katika Simala, I. *Utafiti wa Kiswahili*. Umoja Press

Momanyi, C. (1998). "Usawiri wa Mwanamke Mwislamu Katika Jamii ya Waswahili kama Inavyobainika Katika Ushairi wa Kiswahili". Tasnifu ya PHD, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Muniu, G. (2013). "Ujagina wa Mwanamke Katika Pango". Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mbiti, J. (1969). African Religions and Philosophy. Oxford: Heinneman Educational Publishers

Mwangi, E. (2009). Violence, Sex and Hip-hop Hype. *Sunday Nation,* Nairobi: Nation Media Group. Toleo la 20.09.2009

Nyariki, E. (2014). Mtoto wa Kike Katika 'Kidagaa Kimemwozea'. *Taifa Leo,* Nairobi: Nation Media Group. Toleo la 14.02.2014

Okunna, C. (1995). "Small Participatory Media Technology as an Agent of Social Change in Nigeria: Implications for the Status of Women in the Society". Africa Media Review. Vol. 6, No.1 uk.45- 58

Okunna, C. (1992). "Female Faculty in Journalism Education in Nigeria: implications for the Status of Women in the Society". Africa Medaia Review. Vol. 17, UK. 45-58

Pilcher, J na Imelda W. (2004). 50 Key Concepts in Gender Studies. Los Angeles: Sage Publication

Stacy, R. (1997). Defamiliarization in Language and Literature. Syracuse: Syracuse University Press.

Wafula, R. na Kimani, N. (2007). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K. (2017). "Wanariwaya wa Kike Mpo Wapi. *Taifa Leo*, Nairobi: Nation Media Group. Toleo la 23.03.2017

Wood, J. (2013). Gendered Media: The influence of Media on Views of Gender. http://www.nyu.edu/classes/jackson/causes.of.gende.rinequality